

OFISA YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE

SHULE YA SEKONDARI BUKONGO.



SIMU: 0754810701 au 0758115413

S L.P. 474,

Email: domairamusa @gmail.com

NANSIO-UKEREWE.

10 / 06 /2017

NDUGU

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2017/2018

Ninayo furaha kubwa kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na **Kidato cha Tano** katika **Shule ya Sekondari Bukongo** iliyopo Wilayani **Ukerewe**, Mkoa wa **Mwanza**.

Kwa kuwa wewe ni mmoja miongoni mwa wachache **waliobahatika** kuchaguliwa kuendelea na masomo ya juu ya sekondari, ni imani yangu kuwa utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa kusoma kwa bidii kwa manufaa yako binafsi, familia yako na taifa kwa ujumla.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Bukongo ipo kilomita mbili (2) nje kidogo ya mji mdogo wa Nansio kwa upande wa Kaskazini, ni mwendo wa kama dakika kumi kwa usafiri wa gari kutoka bandari ya Nansio au dakika tano kutoka kituo cha mabasi cha Nansio.

Usafiri kufika Mjini Nansio ni wa meli kama utatokea Mwanza mjini, na kama utatokea Bunda mkoa wa Mara, utapanda magari yanayotoka Bunda mpaka Nansio kupitia kivuko cha Kisorya.

KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 17/07/2017 na masomo yataanza mara moja na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/07/2017. Iwapo hutaripoti hadi tarehe hiyo utahesabiwa kuwa umekataa nafasi uliyopewa, hivyo nafasi itahesabiwa kuwa wazi na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za serikali.

